

KENYA MUSIC FESTIVAL FOUNDATION
Music and Elocution Proficiency Course, 1996

MSHAIRI, USHAIRI NA JAMII

Mhadhara wa

KITHAKA WA MBERIA

Umetolewa

Senior Chief Koinange High School

April 23, 1996

MSHAIRI, USHAIRI NA JAMII

na

Kithaka wa Mberia

1. Maelezo ya Ushairi

Ushairi ni utanzu wa fasihi unaotumia lugha kwa kuichuja na kuipangilia kwa namna maalum. Huo mchujo na mpangilio maalumu unaipa lugha ya kishairi upya, uzito wa maana, mdundo au mziki, uchache wa msamiati, ladha masikioni, mguso kwenye hisia na urahisi wa kukumbukika.

Kupitia utungo wa kishairi, mtunzi huwa na nafasi wa kuwasilisha mawazo, hisia, tajriba, dhana, au msimamo wake kwa lugha ya mkato na yenye athari kwenye hisia za msikilizaji au msomaji.

2. Lugha katika Ushairi

Lugha ni sehemu mojawapo ya malighafi katika ushairi. Kwa sababu hii, mshairi hana budi kuimudu vilivyo lugha anayoitumia. Kwa mfano, akiwa mtunzi anayetumia Kiswahili, inambidi kufahamu barabara vipengele mbalimbali vya lugha hii. Inamlazimu kuelewa vizuri sarufi yake na kuwa na utajiri mkubwa wa msamiati.

Kuna njia mbalimbali ambazo mshairi anaweza kutumia ili kukuza uwezo wake wa lugha. Miongoni mwa njia hizi ni kusoma vitabu vingi vya fasihi ambavyo vimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Mtunzi pia ataweza kupanua uwezo wake wa lugha ya Kiswahili kwa kukizungumza na kukitumia katika maandishi katika maisha ya kila siku.

3. Ilhamu

Kwa kawaida, mshairi hutunga shairi baada ya kujiwa na ilhamu. Ilhamu ni mguso au msukumo **katika** Mguso au msukumo huu unaweza kutokana na wazo akilini mwa mshairi. Pia unaweza kumjia kutokana na tukio linalomhusu au ambalo ameshuhudia. Ilhamu inaweza kumjia baada ya kugusa, kunusa, kuona, kusikia au kupata ladha fulani kinywani. Pia inaweza kumjia baada ya kusoma kitabu au gazeti, kusikiza redio au kutazama televisheni.

Tunaweza kuongeza uwezekano wa kujiwa na ilhamu kwa kutia hisia zetu makali kimaksudi. Tunaweza kutia hisia makali, kwa mfano, kwa kujifunza na kujizoeshwa kutazama na kusikiza kwa makini na kujaribu kufasiri tunayoyaona na kuyasikia. Tunaweza pia kuongeza uwezekano wa kujiwa na ilhamu kwa kushiriki kwenye vipengele vingi vya maisha, kusafiri na kutangamana na watu wa makundi mbalimbali.

4. Umuzi wa aina ya shairi

Ushairi una miundo mingi. Baada ya kujiwa na ilhamu inabidi mshairi aamue muundo wa shairi atakaotumia katika utungo wake. Itambidi aamue kama atatumia muundo wa ushairi-jadi, ushairi-huru au hata ushairi-picha. Akiamua kutumia muundo wa ushairi-jadi itamlazimu kuchagua mojawapo ya bahari mbalimbali za ushairi huo. Kwa mfano, anaweza kutumia takhmisa (utano), tarbia (unne), tathlitha (utatu) au tathnithza (uwili).

Ikiwa mtunzi ataamua kutumia muundo wa ushairi-huru au ushairi-picha hana budi, kukumbuka kwamba tofauti baina ya ushairi-jadi kwa upande mmoja na ushairi-huru na ushairi-picha kwa upande wa pili imo kwenye suala la vina, mizani na uakifishi unaohusiana na vina na mizani. Ushairi-jadi una sifa hizo ilhali ushairi-huru na ushairi-picha hauna. Sifa nyingine za ushairi zinapatikana katika aina zote za mashairi. Kwa mfano, mashairi ya aina zote yanatarajiwa kuwa na lugha yenye ladha, uzito wa maana, upya, iliyochujwa, na yenye mdundo maalum. Mtunzi asichague kutumia ushairi-huru au ushairi-picha akidhania kuwa hiyo itakuwa njia ya mkato ya kufikia malengo yake ya utunzi. Ili lugha ya utungo wake iwe ya kishairi, itamlazimu atumie mbinu kama vile jazanda, tashibihi, tashihisi, balagha, chuku, litifati, tadmini, **tasfida**, mafumbo, kejeli, usambamba, ukinzani, tashtiti, takiriri na majazi. Asipofanya hivyo, utungo wake hautakuwa shairi bali lugha ya kawaida ambayo imepangwa kama shairi.

5. Utunzi na Ukuaji wa Shairi

Wakati wa kutunga, inampasa mshairi kutumia mbinu za utunzi kwa namna ambayo itamwezesha kupata utungo **wenye** mzuri wa lugha na mawazo. Anapaswa kutumia msamiati au lugha kwa jumla kwa namna ambayo itaupata utungo mtiririko mzuri wa mawazo na ujumbe ambao umekamilika. Isitoshe, itakuwa muhimu lugha yake iweze kusababisha hali fulani ya hisia kwenye akili ya msomaji au msikilizaji.

Baada ya kutunga shairi, ni vizuri kulipa nafasi ya kukua. Njia ya kutimiza jambo hili ni kulisoma shairi mara kadha wa kadha ili kulifanyia mageuzo ya kuliboresha. Huku kulisoma shairi na kulifanyia mageuzo kunaweza kuchukua siku kadha wa kadha, miezi au hata miaka. Muda unaochukuliwa na shairi ili kukua na kukomaa unategemea shairi linalohusika. Baadhi ya mashairi yanachukua muda mrefu kuliko mashairi mengine. Kwa jumla, shairi ambalo linatokana na ilhamu iliyojaa litachukua muda mfupi kukua na kukoma. Linaweza kuchukua siku chache au hata siku moja. Kwa upande mwingine, shairi ambalo limetungwa huku mshairi na mguso au msukumo wa kiwango cha chini, litachukua muda mrefu kuimarika na kufikia ukomavu.

Ili kuchunguza na kuboresha mdundo wa shairi, ni vizuri kulisoma kwa sauti na kwa mpigo imara. Jambo hili litatambulisha mishororo inayohitaji kurefushwa na ile inayofaa kufupishwa.

6. Mshairi na Jamii

Ushairi unaweza kutumiwa kubadilisha mtazamo kuhusu jambo fulani. Shairi linaweza kugeza tabia au mienendo ya watu. Ukweli huu unampa mshairi nafasi ya kuchangia katika maendeleo ya jamii. Kwa mfano, anaweza kutunga mashairi kuhusu masuala muhimu kama vile haki za binadamu, nafasi ya mwanamke katika jamii, ufahamu wa maradhi na namna ya kuepukana nayo, ajali za barabara, na madhara yanayotokana na madawa ya kulevya.

Mshairi hana budi kuhakikisha kwamba sanaa yake haitumiki kwa namna ambayo itadhuru jamii. Mshairi hatanufaisha jamii akitunga, kwa mfano, mashairi yanayosifu ulevi, kupinga unyonyeshaji wa watoto, kuchochea chuki ya kikabila, na kutukuza talaka.

ASANTENI

Prof. Kithaka wa Mberia, PhD, has taught linguistics, Kiswahili and communication in University of Nairobi, Nairobi, Kenya, since 1982. Besides being an academic, he is a poet and a playwright. He has travelled extensive for academic conferences, art festivals. Moreover, besides University of Nairobi, he has taught in universities, namely, Virginia State University (United States of America), University of Warsaw (Poland) and Hankuk University of Foreign

Studies) South Korea. He has published numerous papers and chapters in refereed journals and academic books respectively. His published creative works include: *Mchezo wa Karata* (1997), *Natala* (1997), *Kifo Kisimani* (2001), *Bara Jingine* (2001), *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* (2004), *Redio na Mwezi* (2005), *Msimu wa Tisa* (2007) and *Rangi ya Anga* (2014) and *Doa* (2018). Many of his creative works have been translating and published in English. They are *Death at the Well* (2011), *Natala* (2011), *Flowers in the Morning Sun* (2011), *Another Continent* (2011) and *A Game of Cards* (2011).